

**MAAMUZI MAKUBWA MATATU KATIKA  
MAISHA YAKO**

*“Maamuzi matatu yatakayoamua hatima ya  
maisha yako”*

**DR STANLAUS GEORGE MWANISAWA (MD)**

## UTANGULIZI

Kwa miaka kadhaa sasa nimekuwa nikifuatilia na kujifunza kupitia maisha ya watu wengi bila wao kujua wakiwemo wazazi wangu, baada ya miaka mingi nimefikia hitimisho ya kwamba kuna maamuzi makubwa matatu ambayo ni msingi wa maisha ya mwanadamu.

Maamuzi haya matatu ndiyo yanaamua namna maisha ya mtu yatakavyokuwa kwani yana uwezo wa kubadili kabisa mfumo mzima wa maisha ya mtu.

Nimeona maisha ya watu wengi jinsi yalivyokuwa bora na wengine kuharibiwa kabisa kwa sababu ya maamuzi haya makubwa matatu.

Ukifanya maamuzi haya matatu kwa usahihi utayafurahia maisha yako ya hapa duniani na kuishi kama mbinguni, lakini ukikosea uwe na uhakika maisha yako ya duniani utayaona kama jehanamu.

Maamuzi haya matatu ni muhimu sana kiasi kwamba ukikosea moja kati ya maamuzi haya inaweza kukuvuruga kwenye ufanyaji wa

maamuzi yale mengine mawili na kuharibu kabisa maisha yako. Kwa hiyo kuna haja kubwa ya kuwa makini sana unapofanya maamuzi haya matatu.

Maamuzi hayo matatu ni haya; *Nitamwabudu na kumtumikia nani? nitafanya kazi gani? Na nitamwoa au nitaolewa na nani?*

Mungu amenipa Neema ya kukuandikia kitabu hiki ili uweze kupata maarifa juu ya maamuzi haya na namna yanavyoweza kuathiri maisha yako, lakini pia kukukumbusha umuhimu wa maamuzi haya kwenye maisha yako ili usifanye makosa ambayo wengine wameshayafanya na sasa wanavuna matunda ya maamuzi yao.

Karibu sana katika safari ya kujifunza juu ya maamuzi haya makubwa matatu. Ni imani yangu kwamba utakapomaliza kitabu hiki, utakuwa mtu mwenye maarifa na mtazamo wa tofauti sana juu ya maamuzi haya matatu.